**HOTUBA YA UFUNGUZI ILIYOTOLEWA NA MWENYEKITI WA KAMATI YA UONGOZI, ELIESH LEMA KATIKA UZINDUZI WA MFUKO WA VYOMBO VYA HABARI TANZANIA, TAREHE 3 DESEMBA, 2008. KARIMJEE HALL**

Mheshimiwa Ndugu Samwel Sitta, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mgeni wetu rasmi; Mheshimiwa George Mkuchika, Waziri wa Utamaduni, Habari na Michezo Mheshimiwa Sofia Simba, Waziri katika Ofisi ya Rais, Utawala Bora, Waheshimiwa Mabalozi walio nasi hapa; Mheshimiwa Balozi Adrian Shlapfer, Ubalozi wa Switzerland na Mwakilishi wa Wahisani, Waheshimiwa Wabunge waliopo hapa, Waheshimiwa Wanajamii wa Habari; Waheshimiwa Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana.

Kwa niaba yangu mwenyewe, Kamati ya Uongozi na Sekretariati ya Mfuko wa Vyombo vya Habari Tanzania, nawashukuru sana kwa kuweza kufika kushiriki nasi na kusheherekea tukio hili muhimu – **Uzinduzi wa Mfuko wa Habari Tanzania.** Tukio hili ni sehemu mojawapo ya maendeleo katika sekta ya Habari nchini, ambayo imekuwa, na inaendelea kuweka jitihada kubwa katika kuhabarisha, kuelimisha na kuburudisha umma wa Watanzania.

Sekta ya Habari imekuwa hai kabla na baada ya uhuru, mfano, gazeti la *Tanganyika Standard* lililokuwa likitetea maslahi ya mkoloni na gazeti la *Mwafrika* lililosaidia kueneza harakati dhidi ya ukoloni; na baada ya uhuru, gazeti la *Uhuru* pamoja na *Tanganyika Broadcasting Corporation,* vyombo vilivyofanya kazi kubwa ya kueneza itikadi za kisiasa na kujenga umoja wa nchi.

Sasa, miaka 47 baada ya uhuru, Watanzania waliofikia takriban millioni 40, wanahudumiwa na vyombo vya Habari vinavyofikia magazeti 70, vituo vya redio 45 na vituo vya luninga 27 . Wingi huu wa vyombo vya kuhabarisha watu ni kiashiria kimojawapo cha kuwepo mazingira ya kidemokrasia pamoja na uhuru wa kiasi fulani wa vyombo vya habari.

Katika hali hii ya vuguvugu la maendeleo na nguvu ya mabadiliko katika jamii, watumiaji na wadau wa Habari wanatambua kwamba sharti masuala yaibuke mara moja moja, kuhusu utendaji wa sekta ya Habari, inawezekana masuala muhimu yakaibuka pia katika mdahalo wa Wanahabari mashuhuri utakaofuata baada ya uzinduzi wa Mfuko huu.

Katika muda mchache ujao, tutaona sinema fupi juu ya maoni ya Watanzania wachache kuhusu vyombo vya Habari. Watanzania hawa wa jinsia na umri mbalimbali wanatuhakikishia kuwa vyombo vya Habari ni muhimu kwao, kwani vinawapa habari kuhusu matukio mbalimbali yanayotokea nchi nzima, na muhimu sana, vyombo vya Habari vinaweza kufanya utafiti na kuibua matendo maovu yanayotendeka katika jamii yakichangia katika kufifisha maendeleo ya watu. Jambo hili linaimarisha uwajibikaji na kuimarisha demokrasia. Hata hivyo, wananchi hawa wanatoa hadhari kwa wanahabari kuzingatia UKWELI katika uhabarishaji na uelimishaji, na kwamba visiwe vyombo vya mijini tu bali viwafikie pia watu wa vijijini.

Maoni haya yanalenga kabisa sababu zilizosukuma kuanzishwa kwa Mfuko wa Habari Tanzania. Mfuko huu umeanzishwa kwa msaada wa Wahisani wachache kwa

madhumuni ya kuendeleza hamasa katika sekta ya Habari iliyo huru na yenye utofauti ili iweze kuongeza nguvu katika kufanya utafiti pamoja na kuzingatia habari zenye umuhimu kwa umma. Pia, Wanahabari waweze kutimiza kikamilifu azma yao ya kuhabarisha na kuelimisha umma kwa kutoa habari zenye kina na zilizohakikiwa vema.

Mfuko wa Habari Tanzania utatoa misaada ya fedha kwa ushindani, kwa wanahabari binafsi, Vyombo vya Habari, Mashirika yasiyo ya Kiserikali yaliyo na programu za kutoa habari. Misaada mingine kwa washiriki wote washindi itajumuisha uwezeshaji kwa 'Kujifunza kwa vitendo', kufanya kazi na mshauri pamoja na kushiriki katika mpango wa Jifunze. Mpango huu wa Jifunze, unazingatia kuongeza ubora wa uhabarishaji na utafiti. Kwa hiyo, ushauri utalenga katika ujenzi wa dhana, ubunifu wa mawazo, kuimarisha ubora na kuendeleza mrejesho kutoka kwa watumiaji wa habari. Njia hii inategemewa kuimarisha uwezo wa wanahabari.
Waheshimiwa Wageni wetu, kipengele hiki cha mafunzo kitapewa kipaumbele na Mfuko wa Habari Tanzania kwani ni muhimu sana kwa mradi huu. Mafanikio yake ndiyo yatakayotuhakikishia kuwa stadi watakazopata wanahabari zitakuwa endelevu na hivyo Mfuko huu utakuwa umetimiza lengo lake. Wote tunafahamu kinachotokea kwa miradi mingi baada ya ufadhili kuisha. Lakini tunaamini kwamba kama uwezo na stadi za wanahabari zikiimarika vya kutosha kwa kupitia kazi walizofanya na kujifunza kwa vitendo, basi uhabarishaji bora na wenye kina utaendelea hata baada ya Mfuko kwenda mahali pengine.
Labda sasa tujiulize, je, uhabarishaji bora na uchunguzi wa kina ni upi?

Katika mazingira ya uhuru wa mawazo, watu huruhusiwa kujieleza kwa njia yao. **Mfuko wa Vyombo vya Habari Tanzania** unaelewa uhabarishaji bora na wenye kina kuwa ni ule unaozingatia **UKWELI.** Na ili kufikia ukweli huu, sharti habari iwe imefanyiwa utafiti barabara, mwanahabari awe na uelewa kuhusu jambo analotolea ripoti, sharti athibitishe taarifa kutoka vyanzo vinavyoaminika kadhaa, awe jasiri kuuliza maswali magumu na kisha mwanahabari apambanue na kuhakiki masuala yanayojitokeza. Tunajua kwamba umaskini na athari zake katika maisha yetu ya kila siku hubeba maovu mengi ambayo yatahitaji kuangaliwa. Kwa hiyo, masuala pendwa kama ufisadi yatapata wenza katika habari, na yale mengine kama kashfa na umbeya yanaweza yakajikuta yamekosa nafasi.

Waheshimiwa Wageni wetu, maneno haya mafupi ya utambulisho wa Mfuko wa Habari Tanzania hayataweza kuelezea mambo yote kuhusu Mfuko. Mkutano wa Habari uliofanyika mchana huu, vipeperushi vilivyotolewa, pamoja na kazi itakayofanywa na wanahabari chini ya Mfuko, vitakuwa kielelezo thabiti cha maana na umuhimu wa Mfuko huu.
Kwa idhini yenu, nachukua nafasi hii kuwakaribisha kutazama filamu fupi juu ya maoni ya Watanzania wachache kuhusu vyombo vya habari. Baada ya hapo, nitamkaribisha Balozi Adrian Schlapfer, kuzungumza machache kabla ya kumkaribisha Mheshimiwa Mgeni wetu Rasmi.

Asanteni na Karibuni.